

**Repoti ya Semina ya Usalama Barabarani kwa Wapanda Baisikeli  
Imeendeshwa na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji, Idara ya Usalama Barabarani  
kwa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam (UWABA)  
Jumamosi Tarehe 19 Januari 2008**

Lengo moja la Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam (UWABA) ni kuongeza usalama barabarani kwa wapanda baisikeli, kwa hiyo chama hiki kilitafuta jinsi ya wanachama wake kufundishwa kuhusu sheria za barabara na usalama barabarani kwa wapanda baisikeli. Chuo cha Taifa cha Usafirishaji walikubali kufanya semina kwa wanachama wa UWABA kama huduma ya bure kuelimisha jamii.

Wanachama 21 wa UWABA walifundishwa, ambao ni madereva wa guta, fundi baisikeli na watu wengine wanaotumia baisikeli kama usafiri wa kila siku. Semina hii ilifanyika Chuo cha Usafirishaji Mabibo kutoka saa mbili asubuhi hadi saa nane na nusu mchana jumamosi tarehe 19 Januari 2008.

Washiriki walifundishwa kuhusu sheria na kanuni za usalama barabarani kwa wapanda baisikeli, alama na michoro ya barabarani na uendeshaji baisikeli kwa kujihami. Mafunzo ya muhimu waliyopata yalikuwa kuhakikisha baisikeli ipo kwenye hali nzuri, vipi kuendesha baisikeli kwa usalama barabarani, umuhimu wa uheshima kati ya wanaotumia barabara, haki na wajibu wao kama ajali ikitokea, sheria za barabara, makutano ya barabara, mawasiliano barabarani na maana ya alama za barabara.

Wanachama walishiriki vizuri katika semina kwa kuuliza maswali na kuchangia katika mazungumzo.

Mwisho wanachama wa UWABA walishukuru sana Chuo cha Taifa cha Usafirishaji kwa kutoa hudumu hii nzuri kwa jamii ili kuongeza usalama barabarani kwa wapanda baisikeli. Mkuu wa Idara ya Usalama Barabarani, Bwana Chard Wemba alisema kwamba semina hii ni hatua ya kwanza na Chuo kitapenda kuendelea kushirikiana na UWABA kutoa mafunzo haya kwa wapanda baisikeli wengine.

**Walimu**

C. Wemba – sheria na kanuni za usalama barabarani kwa wapanda baisikeli

C. Kisunga – alama na michoro ya barabarani

H. Mabalwe – uendeshaji baisikeli kwa kujihami

**Washiriki**

Abdallah Khatib	Magomeni	Fundi
Ally Athuman	Mkuranga	Biashara
Ally Saidi Mohamedi	Mabibo	Fundi
Ally Saidi Mwishehe	Tabata	Guta
Ally Salum	Manzese	Guta
Aseli Wilison	Mabibo	Dereva wa Baisikeli
Dominata Rwechungura	Mabibo	Mkulima
Elaine Baker	Magomeni Makuti	System Analyst
Filbert Mbecha	Mabibo	Guta
Frank Peter Rwechungura	Mabibo	Mwanafunzi
Hamadi Hatibu Bwaja	Mabibo	Fundi Baisikeli
Husein Hamza Hamisi	Temeke	Fundi
Juma Ali Salehe Jongo	Manzese	Biashara
Jumanne Idd Selemani	Mabibo	Fundi Baisikeli
Kassim Bakari	Manzese	Guta
Kibwana Mohammad Msiga	Vingunguti	Biashara
Paulo Atibu Hatibu	Keko Mwanga	Biashara
Rahma Ali	Mabibo	Biashara
Ramadhani Rajabu Nyengo	Mburahati	Guta
Rashidi Saidi Karanji	Mabibo	Guta
Yusufu Juma	Mabibo	Dereva Guta